OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI

SHULE YA SEKONDARI GEGEDI
S. L.P. 410
BARIADI - SIMIYU

TAR. ……

Kumb Na. GSS/S3506/JI/2021

JINA LA MWANAFUNZI ……..……

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI GEGEDI MWAKA 2021**

1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari GEGEDI. Shule ipo katika kijiji cha Mwaumatondo, Kata ya Mwaumatondo, Tarafa ya Nkololo, Halmashauri ya wilaya ya BARIADI mkoa wa SIMIYU.

Masomo yanayofundishwa shuleni ni pamoja na Civics, Historia, Geografia, Kiswahili, English, Basic mathematics, Chemistry, Biology na Physics. Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili ambalo linafundishwa kwa lugha ya Kiswahili.

A. ***VYAMA NA VIKUNDI VYA HIARI VYA WANAFUNZ***I.

Shule inavyo vyama vya hiari ambavyo mwanafunzi anaruhusiwa kujiunga kwa malengo ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kielimu. Vyama hivyo ni pamoja na SCAUT, MALIHAI CLUB (kikundi cha mazingira), FEMA CLUB , DEBATE CLUB N.K.

Mwanafunzi anaruhusiwa kujiunga na chama / vyama hivyo kwa hiari akihitaji kufanya hivyo bila kuvunja sheria za shule na nchi kwa ujumla.

Kila kikundi tajwa hapo juu kina walimu walezi hivyo ukifika shuleni utayapata maelekezo na vigezo vya kujiunga na kikundi husika. Karibu sana.

NB; LUGHA YA MAWASILIANO UKIWA SHULENI NI KIINGEREZA TU!

Shule itafunguliwa tarehe **11.01.2021** Saa 1:00 Asubuhi na **unatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo bila kukosa**. Kushindwa kuripoti kwa tarehe tajwa kutapelekea mzazi/mlezi wako kuchukuliwa hatua kali za kisheria ikiwemo kufikishwa mahakamani

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1: Sare ya shule

A. **Wavulana**

i. Suruali ya kaki moja na nyeusi moja. Tai nyeusi moja na kaki.

Aina ya mashono utapewa maekelezo wakati wa kuchukua fomu.

NB: Atakaye shona suruali isiyokuwa na maadili na kwa kiwango hataruhusiwa kuivaa Shuleni

ii. Shati nyeupe mbili mikono mifupi, soksi jozi 2 rangi nyeupe

iii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi 02 vyenye kamba na visiwe na kisigino kirefu.

iv. Tai 02 (rangi ya kaki moja na nyeusi moja)

v. Mkanda wa suruali mweusi – wenye belt ndogo.

vi. Sweta rangi ya blue.

vii. Sare ya michezo ni Bukta rangi ya blue, raba na t - shirt ya blue yenye michilizi mweupe mikononi.

viii. Daftari kubwa 12 (**counter book**), kalamu na seti ya hesabu (mathematical set)

ix. Dictionary ya ENGLISH - ENGLISH.

B. **Wasichana**

i. Sketi kaki moja na nyeusi moja **inayovuka magoti nchi mbili**. Mashono utapewa maelekezo wakati wa kuchukuwa fomu.

NB: - Kitambaa cha **Sketi lazima kiwe kizito**

-Atakayeshona sketi isiyokuwa na maadili na kwa kiwango hataruhusiwa kuivaa shuleni.

ii. Shati nyeupe mikono mifupi, soksi jozi 2 rangi nyeupe zisizo na mapambo ya aina yoyote

iii. Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2 na visiwe na kisigino kirefu.

iv. Sweta rangi ya blue

v. Tai 2 (rangi ya kaki na nyeusi moja)

vi. Sare ya michezo ni tracksut ya blue yenye michilizi mweupe pembeni na raba .

vii. Daftari kubwa 12 (counter book), kalamu na set ya hesabu (mathematical set)

NB: Vazi la hijabu lifanane na sare ya shule

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ambazo zitajazwa kikamilifu kabla ya kuzikabidhi wakati wa kusajiliwa shuleni;

- ❖ Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
- ❖ Fomu ya vipimo vya afya. Ijazwe na mganga wa hospitali ya Serikali. Kwa mwenye matatizo ya kiafya aje na cheti cha daktari kwa uthibitisho ili atambulike shuleni.
- ❖ Fomu ya kuthibitisha uhalali wa mwanafunzi. (**ijazwe na mwalimu mkuu mwenyewe**)
- ❖ Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
- ❖ Sheria na kanuni za shule, zisomwe na kuzingatiwa kwa kila mwanafunzi

KARIBU SANA

`…….

JOSEPH S. CHEYO

MKUU WA SHULE

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

3.1: Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandaishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wa shule, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa kama mwanafunzi katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(i) Kutunza mali za shule na za Umma

3.2. **Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kusimamishwa au kufukuzwa shule**;

(a) Wizi (b) Uasherati na ushoga (c) Ubakaji (d) Kupiga au kupigana
(e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli, n.k
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma (g) Kudharau Bendera ya Taifa (h) Kupata mimba au Kusababisha mimba (i) Kuoa au kuolewa (j) Kutoa mimba (k) Kuwa na simu ya mkononi
(l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki migomo, kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(m) Kukataa adhabu kwa makusudi

Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi;

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

NB: **Tafadhali soma kwa makini Maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU

……

JOSEPH S. CHEYO

MKUU WA SHULE

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GEGEDI

Anuani ----------

Tarehe----------

MKUU WA SHULE
GEGEDI SEKONDARI,
S.L.P 410
BARIADI.

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GEGEDI

Mimi .....ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule yako, nakubali kujiunga na shule hii. Naahidi kuwa nitakuwa mwaminifu, mtiifu, nitafuata sheria na taratibu zote za shule, nitatunza mali zote za umma zilizopo shuleni, nitasoma na kufanya kazi zote za shule kwa uwezo wangu wote na nitaishi kwa amani na kujiheshimu katika jumuiya ya shule na jumuiya inayoizunguka shule.

Sahihi ya mwanafunzi

Mimi .....
Mzazi / Mlezi wa.....mwanafunzi wa shule ya Sekondari Gegedi, Naahidi kuwa:-

(i) Mtoto wangu atafika shuleni na vifaa vyote alivyoagizwa na shule
(ii) Kwa kipindi chote mtoto wangu atakapokuwa mwanafunzi wa shuleni nitashirikiana na jumuiya ya shule kumpatia taratibu za shule.
(iii) Mtoto wangu awapo nyumbani nitampatia muda na mazingira mazuri ya kujifunzia na kufanya mazoezi aliyopewa na waalimu wake (Home work) na nitamueleza pale nitakapoweza.
(iv) Nitawajulisha waalimu mara moja mabadiliko yoyote mabaya katika tabia ya mtoto wangu.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, AND TECHNOLOGY

GEGEDI SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 410,
BARIADI.
DATE…….

THE MEDICAL OFFICER,
……,
P.O.BOX ……
BARIADI.

RE: MEDICAL EXAMINATION.

Please examine the under mentioned boy/girl as his/her fitness for studies at this school.(This form should be completed by a Government Medical Officer).

Students full name: ----------
Blood test ----------
Stool Examination: ----------
T.S.test: ----------
Asthma: - ----------
Eye disorder: ----------
Nose disorder: ----------
Skin disorder: ----------
Anaemia : ----------
Chest: - ----------
Operation: ----------
Serious Accidents: ----------
Any other infections disease: ----------
Pregnancy: ----------

ADDITIONAL INFORMATION (eg.physical defects or impairments)
Infections chronic of Family disease etc:

I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE STUDIES AS INDICATED ABOVE.

Signature: ----------
Designation: ----------
Station: - ----------
Date: ----------